

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
UTARATIBU WA KUMWONDOA RAIS MADARAKANI

Taarifa
ya
Hoja

107.-(1) Mbunge yeyote aweza kuwasilisha kwa Spika taarifa ya Hoja ya kutaka kumshtaki Rais endapo taarifa hiyo itakuwa imetiwa saini na Wabunge wasiopungua asilimia ishirini ya Wabunge wote kwa mujibu wa Ibara ya 46A ya Katiba.

(2) Endapo Spika ataridhika kuwa hoja ya kumshtaki Rais imetimiza masharti ya Katiba, ataruhusu mtoa hoja kuwasilisha Bungeni

hoja ya kupendekeza kwamba Kamati Maalum ya Uchunguzi iundwe ili isikilize shauri la kumshtaki Rais.

(3) Hoja ya kutaka kuunda Kamati Maalum ya Uchunguzi itaamuliwa bila mabadiliko wala mjadala wowote, na uamuzi wa Bunge utafanywa kwa kuzingatia masharti ya Katiba, na utafanywa kwa kura za siri.

108. Endapo hoja hiyo itakuwa imeafikiwa, Spika, atateua Wajumbe saba kutoka miongoni mwa Wabunge kwa kuzingatia uwiano wa uwakilishi wa Vyama vya Siasa Bungeni.

109.-(1) Kamati Maalum ya Uchunguzi itaweka utaratibu wake wa kufanya kazi kwa mujibu wa Katiba, Kanuni hizi na Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge ya Mwaka 1988.

(2) Spika aweza kuiwekea Kamati Maalum ya Uchunguzi muda maalum ambamo Kamati hiyo itatakiwa kukamilisha kazi yake na kutoa taarifa Bungeni.

(3) Kiwango cha mkutano wowote wa Kamati Maalum ya Uchunguzi kitakuwa ni Mwenyekiti, Jaji Mkuu wa Tanzania, Zanzibar na Wajumbe wengine wanne.

110. -(1) Endapo kwa mujibu wa Orodha ya Shughuli za Bunge utafika wakati wa Bunge kujadili taarifa ya Kamati hiyo Maalum ya Uchunguzi basi Bunge litaingia katika Kamati ya Bunge Zima ili kushughulikia taarifa hiyo. Bunge laweza kumruhusu Mwenyekiti wa Kamati Maalum ya Uchunguzi kuwasilisha na kuelezea uamuzi wa Kamati yake kwenye Kamati ya Bunge Zima.

(2) Wakati Bunge likiwa katika Kamati ya Bunge Zima kushughulikia mashtaka dhidi ya Rais, mtuhumiwa atakuwa na fursa ya kuingia katika Kamati hiyo na kujieleza kuhusu mashtaka dhidi yake.

(3) Baada ya Kamati ya Bunge Zima kukamilisha kazi zake na Bunge kurudia, mtoa hoja atatoa taarifa ya ukamilishaji wa shughuli za Kamati ya Bunge Zima na kama mashtaka dhidi yake yatakuwa yameonekana kuwa yana msingi papo hapo atatoa hoja kwamba Bunge lipitishie azimio la kumwondoa Rais madarakani kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 56A(5) ya Katiba.

Wajumbe
wa
Kamati
Maalum
ya
Uchu-
nguzi
Utaratibu
wa Kazi

Utaratibu
katika
Kamati ya
Bunge
Zima
kuhusu
Mashtaka
dhidi ya
Rais

Azimio
la
Kumwo-
ndoa
Rais